


MRADI WA KUSAIDIA KUTABIRI MAGONJWA YA MLIPUKO KWA KUTUMIA MIFUMO YA AKILI MNEMBO WAZINDULIWA MANISPAA YA MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imezindua mradi wa ukusanyaji taarifa (data) zitakazotumika kwa ajili ya kutabiri magonjwa ya mlipuko yanayoambukizwa kwa njia ya maji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia Akili Mnembo (Artificial Intelligence).



Mradi huu unatekelezwa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.



Akizungumza katika utambulisho wa mradi huo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, ndugu Ally Machela, amesema amefurahi kuona watafiti wanaenda kwenye maeneo yenye changamoto na kuwekeza huko ili waone hali halisi.



"Tunawashukuru sana Watafiti wetu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) kwa kuja na mfumo huu mzuri tunaotazamia utakuwa na tija katika Halmshauri yetu ya Morogoro " amesema Machela.



Kwa upande wa Msimamizi wa mradi huo kutoka SUA, Dkt. Neema Lyimo, amesema kuwa mradi huo utakuwa ni suluhisho la kupata taarifa (data) za visababishi vya magonjwa ya mlipuko yanayoambukizwa kwa njia ya maji kama vile homa ya

matumbo (typhoid), amoeba na kuhara, yanayosababishwa na athari za mabadiliko ya tabia nchi.



"Nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na athari za mabadiliko ya tabia nchi hivyo kama wataalamu kwa kushirikiana na watafiti wenzangu tuliona umuhimu wake na kupendekeza utafiti wa kukusanya taarifa juu ya magonjwa ya mlipuko yanayosababishwa na vimelea vya kwenye maji, hasa wakati huu wa mabadiliko ya tabianchi" Amesema Dkt. Lyimo.

Utambulisho wa mradi huu umehudhuriwa na Dr. Charles Mkumbachepa (Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro) , Martin Mzuwanda (Kaimu Afisa Afya wa Manispaa ya Morogoro) na Hezron Ligala (Mratibu wa mfumo wa taarifa za Kinga -NISMIS kutoka Manispaa ya Morogoro).

MWISHO